

Toleo la. 12

Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025



ALIAHIDI | AMETEKLEZA | APEWE TENA 5 | 11 SEPTEMBER, 2020

KASI YA MAGUFULI... HAWATAWEZA!



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



MIKA MITANO TENA KWA MAGUFULI KUKIPAISHA KILIMO

Na Mwandishi Wetu - DODOMA

Chama cha Mapinduzi (CCM) chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wake, Dkt. John Pombe Magufuli, ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kimedhamiria kuendeleza mapinduzi makubwa katika kilimo katika kipindi cha miaka mitano ijayo ili kuhakikisha kinakuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia ya kisasa.

Kwa mujibu wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020- 2025 ambapo Dkt. Magufuli ndiye Jemedari Mkuu wa utekelezaji wake, imeeleza kuwa Chama kitahakikisha kuwa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) inaendelea kutekelezwa na kutoa mchango mkubwa katika usalama wa chakula na, pato la Taifa, maendeleo ya Sekta ya Viwanda na huduma.

“Kuongeza eneo lenye miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta

561,383 mpaka kufikia hekta milioni 1,200,000 ifikapo mwaka 2025 na kuongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta laki 111,192 kwa kukamilisha ujenzi wa skimu za umwagiliaji 261 katika mikoa 25. Kati ya hizo, skimu ndogo ni 179, skimu za kati 63 na skimu kubwa 19”, inaeleza sehemu ya Ilani hiyo ya CCM.

Aidha, skimu mpya za umwagiliaji 208 zitajengwa na kati ya hizo skimu ndogo ni 123, skimu za kati 63, na skimu kubwa 22. Ujenzi huo unatarajia kuongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 136,928 na kwamba sekta binafsi itahamasishwa kushiriki kwenye ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji itakayoongeza eneo la umwagiliaji kwa eka 150,000.

Chama cha Mapinduzi (CCM) chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wake, Dkt. John Pombe Magufuli, ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,



kimedhamiria kuendeleza mapinduzi makubwa katika kilimo katika kipindi cha miaka mitano ijayo ili kuhakikisha kinakuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia ya kisasa.

Kwa mujibu wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020- 2025 ambapo Dkt. Magufuli ndiye Jemedari Mkuu wa utekelezaji wake, imeeleza kuwa Chama kitahakikisha kuwa Programu ya Kuen-deleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) inaendelea kutekelezwa na kutoa mchango mkubwa katika usalama wa chakula na, pato la Taifa, maendeleo ya Sekta ya Viwanda na huduma.

Hatua nyingine zitakazochukuliwa ni pamoja na kujenga na kuimarishwa kwa mabwawa ya uvunaji wa maji ya mvua 88 katika skimu za umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha mpunga na mazao mengine katika mikoa 25 ili kuongeza maeneo ya kilimo cha umwagiliaji.

Pia ilani imeelekeza kuwa itajengwa skimu ya umwagiliaji ya hekta 60,000 kwa kutumia fursa ya Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) na kuwawezesha wakulima kutumia teknolojia na miundombinu ya kisasa za kilimo endelevu na chenye tija kwa njia ya kilimo mseto (Agroforestry) kwenye mazao ya parachichi, korosho, miembe, michungwa, michikichi, minazi na mazao mengine ya miti.

“Kuongeza usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na mbegu bora, mbolea, viuatilifu na zana bora za kilimo kwa kuongeza upatikanaji wa mbolea kutoka tani 586,604 mwaka 2019/2020 hadi tani 800,000 mwaka 2020 hadi 2025.



CHANGAMOTO YA MAJI TANDAHIMBA YAPATIWA UFUMBUZI

Na Mwandishi Wetu - **Tandahimba - MTWARA**

Wananchi wa Jimbo la Tandahimba mkoani Mtwara wamehakikishiwa kuwa changamoto ya upatikanaji wa maji itageuka kuwa historia katika miaka mitano ijayo ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Mgombea wa kiti hicho kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mgombea Mwenza wa kiti cha Urais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ametoa ahadi hiyo leo katika mkutano wa kampeni uliofanyika wilaya ya Tandahimba.

“Awamu ya kwanza ya ujenzi wa mradi wa maji Mpwiti umefikia asilimia 53, awamu zote mbili zikikamilika vijiji 41 vitanufaika na mradi huo”, ameeleza Mhe. Samia.

Akifafanua zaidi, Mhe. Samia amesema kuwa katika suala la kuleta maendeleo, Chama cha Mapinduzi hakina mbadala na kitaendelea kutekeleza jukumu hilo ili kuleta maendeleo kwa wananchi hasa wanyonge.

“Kwa upande wa elimu amesema kuwa shilingi bilioni 6.5 zimepelekwa Tandahimba kugharamia elimu bila malipo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Tunawahakikishia kuwa tutaendelea kutekeleza mpango wa elimu bila malipo kama ilivyo sasa. Pia tutaendelea kuongeza fedha nyingi kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu”, amesisitiza Mhe. Samia.



CCM INAFANYA KAMPENI KISANYANSI

• Yazidi Kukubalika kwa Wananchi

Na Mwandishi Wetu - **GEITA**

Kampeni za Chama Cha Mapinduzi (CCM) zimetajwa kufanyika kisanyansi na kwa weledi wa hali ya juu inayokipa chama hicho fursa ya kukubalika kwa wananchi na kuen-delea kuongoza kwa muhula wa pili wa awamu ya tano.

Hayo yamesemwa leo na Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi Humphrey Polepole katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Chato mkoani Geita ambapo amesema kwamba kampeni za Chama hicho zinafanyika kwa weledi mkubwa.

“Hatutumii usafiri wa anga bali tunatumia usafiri wa barabara ili tuwafikie wananchi wa kila Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata, Kijiji na Mtaa, kwani hawa ndio waliotupa ridhaa ya kuongoza na kwa hali hii hawa ndio watakaotuwezesha kupata ushindi wa kishindo,” amesisitiza Polepole.

Akifafanua zaidi, Ndg. PolePole amesema kuwa Chama hicho kina uhakika wa kuung-wa mkono na wanachama wake zaidi ya mil-ioni 17 na wananchi wasio na vyama kwani wameguswa na jinsi CCM ilivyotekeleza ahadi zake kwa wananchi, jambo litakalosa-bisha kipate ushindi wa kishindo katika uch-aguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

“Kama kura zikipigwa leo, Dkt. John Pombe Magufuli atashinda kwa zaidi ya asilimia 85 kwa sababu watanzania wengi wamemuele-wa na wanamuunga mkono bila kujali itikadi zao,” ameeleza Polepole.

Polepole amekumbushia namna Serikali ya Awamu ya Tano ilivyofanikiwa kudhibiti mfumuko wa bei na hivyo kuwawezesha wananchi kupata maendeleo makubwa katika maeneo wanayoishi.



WAPUUZENI WANASIASA WANAOFANYA UPOTOSHAJI - POLEPOLE

Na Mwandishi Wetu - **GEITA**

Wananchi wametahadharishwa kuepuka wanasiasa wababaishaji, waongo na wanaolin-da maslahi ya mabeberu huku wakitumia lugha za matusi wakati wa kampeni za kuomba kura katika ngazi ya Urais, Ubunge na Udiwani.

Kauli hiyo imetoletwa leo mjini Chato mkoani Geita na Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi Humphrey Polepole wakati wa mkutano na waandishi wa habari kuelezea maendeleo ya kampeni za Chama hicho zinazoendelea katika mikoa ya kanda ya Ziwa.

Akifafanua amesema kuwa baadhi ya wanasiasa hao wanaonekana kuishiwa hoja za msingi katika kuomba kura kwa wananchi hivyo kuamua kuendelea na majukumu mengine baada ya kuona nguvu iliyowekezwa na CCM katika kufanya kampeni.

"Mgombea mmoja aliwafukuza waandishi wa habari katika mkutano wao wa hadhara na kutoa maneno yasiyofaa na mgombea mwingine ameonekana akiondoka nchini kuelekea nchi fulani baada ya kufanya kampeni katika mkoa mmoja tu hali inayoonesha kuwa amekubali kushindwa", amesisitiza Polepole.

Chama chetu kimepeleka makada waandamizi katika kanda mbalimbali ili wasaidie katika kufanya kampeni za kisayansi na kueleza utekelezaji wa Serikali kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na ahadi za CCM kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Chama cha Mapinduzi kimeemdelea kuaminika na wananchi katika maeneo mbalimbali hapa nchini na hata mgombea wake na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kuchaguliwa na wananchi na kuendelea kupata uungwaji mkono katika kila kona anayofika kuomba ridhaa yakuongoza kwa awamu ya pili.

5 KALI ZA CHAMA CHA MAPINDUZI

Sekta ya Kilimo

01

Katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020, Serikali kupitia Chama cha Mapinduzi kiliwaidhinishia ardhi wananchi wa vijiji 1,920 kati ya 1,975 vilivyokuwa ndani ya maeneo ya hifadhi ili kuwaongezea maeneo ya kilimo.

02

Jumla ya Vyama vya Ushirika 16 vya wabanguaji wadogo wa korosho vimeimarishwa na kuweza kuuza korosho tani 291,329 katika nchi za India, China na Vietnam. Aidha, vyama 63 vinauyozalisha ufuta na kokoa vimeunganishwa na kuweza kuuza mazao yake kupitia mfumo wa Soko la Bidhaa.

03


Katika kipindi kinachokuja, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 imejipanga kuongeza upatikanaji wa mbolea kutoka Tani 586,604 mwaka 2019/20 hadi tani 800,000 mwaka 2020/2025.

04

Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 imejipanga kuongeza uzalishaji wa mbegu kutoka tani 71,000 hadi tani 140,000 na kupunguza bei ya mbegu na kutekeleza mikakati ya kuwafikishia wakulima kwa wakati ifikapo mwaka 2025.

05

Katika miaka mitano ijayo (2020/2025), Chama cha Mapinduzi kitahakikisha kuwa Program ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) inaendelea kutekelezwa na kutoa mchango mkubwa katika usalama wa chakula, Pato la Taiifa, maendeleo ya Sekta ya Viwanda na huduma.



WANANCHI, WASOMI WAMUUNGA MKONO RAIS MAGUFULI

• Wasema Anafanya Siasa za Kiungwana, Mwadilifu

Na Mwandishi Wetu

Wananchi waadilifu na wasomi huru wamemuelezea Mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, kama kiongozi anayefuata maadili ya kisiasa na siasa bora kwa kuwa amekuwa akiongea ukweli.

Wananchi hao akiwemo Bw. Jumanne Kikoti mkazi wa Kikuyu, Dodoma amesema kuwa, Rais Magufuli, amekuwa siyo mlaghai na siku zote amekuwa akiwaambia wananchi ukweli hata kama ukweli huo unauma tofauti na viongozi wengine ambao wamekuwa wakitoa ahadi za uongo kwa lengo la kupata kura.

“Rais Magufuli ni muadilifu na anafuata maadili ya kisiasa na siasa bora. Hapendi kudanganya na unaona kabisa anavyoumia pale anapona viongozi wanawadanganya wananchi au hata wanapothubutu kumdanganya yeye linapokuja suala lenye maslahi mapana ya nchi,” anasisitiza Bw. Kikoti.

“Nimesikia mgombea mmoja wa Urais akisema kwamba atawalipa fidia wananchi wote waliovunjiwa nyumba zao kupisha upanuzi wa barabara. Huyu mwanasiasa ni muongo na anawalaghai wananchi kwasababu walijenga katika hifadhi ya barabara kinyume na sheria. Sasa wanasiasa kama hawa sio wa kuwaamini hata kidogo maana wanatoa matumaini ya uongo.” anaeleza Jonathan Makundi wa Kimara jijini Dar es Salaam na kuwasihi wapiga kura kuwa makini na wanasiasa wa aina hiyo.

Mataalam wa Sayansi ya Siasa kutoka Chuo Kikuu cha UDOM na Mkuu wa Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma wa Chuo hicho, Dokta Ajali Nguyahambi, yeye anasema wanasiasa wanapaswa kuwa wakweli mbele ya wananchi ili kufanya siasa safi na za kiungwana.

“Unaweza kuona namna Kiongozi huyu alivyo mkweli na mfuasi wa Maadili ya Kisiasa na Siasa Bora na viongozi wa namna hii duniani nadhani amebaki yeye tu”, anasisitiza Dkt. Nguyahambi na kutoa wito kwa viongozi wote na wagombea kutoa ahadi za kiungwana zinazotekelezeka.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**